

# Kupata usaidizi wakati mtoto wako anapoonewa kwenye mtandao

**Uonevu kwenye mtandao - au unyanyasaji kwenye mtandao – ni wakati mtu aliye kwenye mtandao anapokufanyia ubaya au anamfanya mtu ajihisi vibaya au afadhaike, au hata kumtisha.** Inaweza kutokea kwa watoto kwenye tovuti ya mitandao ya kijamii, mchezo iliyo kwenye mtandao, programu au huduma zingine kwenye mtandao.

Mtu anaweza kumfanya mtoto wako ajihisi vibaya au kukasirishwa na:

- kutuma ujumbe wa kuumiza unaowahusu
- kushiriki picha au video zao za aibu
- kueneza uvumi mbaya kwenye mtandao kuwahusu
- kuwaacha nje ya gumzo la kikundi kwenye mtandao
- kutoa maoni ya ubaguzi yanayowahusu au tamaduni zao.

Uonevu kwenye mtandao unaweza kutokea mtu yeyote. Ni muhimu kwamba mtoto wako ajue kwamba anaweza kuja kwako au mtu mzima anayemwamini ili kupata usaidizi, na asipate shida.

## Kumsaidia mtoto wako akidhulumiwa kwenye mtandao


Kamamtoto wako anaonekana kuwa na wasiwasi au ana wasiwasi kuhusu simu, kompyuta au kifaa chake, waulize kuhusu kinachoendelea.

Mwambie mtoto wako kuwa hakuna mtu anayestahili kuumizwa anapokuwa kwenye mtandao na kuwa ni sawa kuhisi hasira. Ikiwa hawawezi kutatua suala hilo peke yao, wewe unaweza kuwasaidia.

Mara nyingi watoto huenda kwenye mtandao ili kutafuta usaidizi wakati mambo yanapoharibika, kwa hivyo si vyema kila mara kuchukua kifaa chao ili kujaribu kurekebisha mambo.

## Kuripoti unyanyasaji unaotokea kwenye mtandao

1. Kukusanya ushahidi. Piga picha ya skrini yenye maudhui hatari, anwani ya ukurasa wa tovuti (URL) pamoja na jina lenye kutumia kwenye akaunti.
2. Toa ripoti kwa huduma iliyo kwenye mtandao. Mwongozo wa eSafety Guide unaweza kukusaidia kufanya hivi. Ikiwa huduma haitajibu ndani ya saa 48, nenda kwa [esafety.gov.au](http://esafety.gov.au) na bonyeza sehemu ya kifungo cha 'kutaarifu unyanyasaji' chekundu.
3. Zuia mawasiliano zaidi. Tumia mipangilio ili kupuuza, kunyamazisha au kumzuia mtu mwingine na kuangalia mipangilio yako ya faragha.
4. Pata msaada zaidi. Zungumza na mtu mzima unayemwamini au mshauri katika Kids Helpline (1800 55 1800) au headspace.



Kwa maelezo zaidi kuhusu jinsi ya kuweka familia yako salama wanapokuwa kwenye mtandao, tafuta eSafety kwa Wazazi kwenye tovuti yetu.